



Mafunzo ya Biblia

2 Yohana

2 Yohana

Mtume Yohana aliandika Injili, nyaraka tatu na kitabu cha Ufunuo. Waraka wa pili wa Yohana umeandikwa kwa kanisa ambalo hatujui jina lake lakini mandhari ni sawa na maandishi mengine ya Yohana.

Yohana 'Mzee'

Yohana alikuwa mtume na mwandishi mwenye nguvu sana lakini anajitaja mwenyewe katika barua hii kama 'Mzee'. Moyo wa Yohana ulipaswa kuwa kama baba kwa makanisa mengine, kwa unyenyekevu akiwaongoza na kuwaongoza watu wa Mungu.

Kwa 'Mwanamke Mteule'

Haieleweki Yohana anamuandikia nani huu waraka. Huenda ni mwanamke aliye na familia lakini pia kuna uwezekano kuwa anamaanisha kanisa na kwamba watoto ni washiriki. Yohana analipenda hili kanisa na anafurahia katika ukweli wa Mungu ambao unaonekana miongoni mwao.

Salamu za Utangulizi

Marejeleo ya neema, huruma na amani ni vipawa muhimu vitatu vinavyo jitokeza Mungu Baba na Mungu Mwana wanatuletea. Tunashukuru sana neema ya Mungu, kwa sababu tunastahili kutarajia hukumu kutoka kwa Mungu Mtakatifu lakini ametuonyesha huruma, kwa kumruhuzu Kristo kuchukua hukumu ambayo tunastahili kupokea, na utajiri tulio nao ndani ya Kristo, haina hesabu. Tuko na mengi kwa sababu ya neema na huruma za Mungu na amani ya Mungu iko katika mioyo yetu, hata kama hali zinazo tuzunguka zimejaa shida.

Kutembea Katika Ukweli

Yohana anafurahia kuona watu wa Mungu wakitembea katika ukweli. Ana wasiwasi juu ya uzushi na mafundisho ya uwongo, haswa juu ya Kristo, kwa hivyo watu wanaomheshimu Yesu kwa jinsi alivyo kweli watakuwa wa kipekee sana kwa Yohana na, kwa kweli, kwa Mungu. Yesu alitupa amri ys kipendana mmoja kwa mwingine na hili ndilo himizo la Yohana kwa waaminio. Tunapo tembea kwa utiifu kwa amri ya Yesu, kuna kitu cha kipekee juu yetu!

Jihadharini na Mafundisho ya Uwongo

Yohana anafahamu mafunzo ya uongo na potovu na anaelezea tabia kama hizo kuwa 'wapinga Kristo'. Anawahimiza watu wa Mungu wawe na subira na kukimbia mbio za Kikristo kulingana na Mungu. Watu wa Mungu walijulikana sana kwa ukarimu wao lakini Yohana anaonya kanisa hili kutopokea watu ambao hawamuashimu Yesu katika mafunzo yao. Hii ingekuwa tofauti kubwa kwa waumini, ambao kwa asili wangukuwa na mwelekeo wa kumkaribisha kila mtu.

Maneno ya Mwisho

Yohana anajua thamani ya kuwaandikia lakini anafurahia katika tumaini ya kwamba atakutana nao uso kwa uso. Pia anawalettea salamu kutoka kanisa lingine ili kuwatia moyo.

Vipengele vya Kuzingatia:

1. Ukweli ulikuwa wa muhimu kwa Yohana. Ni kwa njia gani ukweli ni wa muhimu katika huduma yetu?
2. Yohana anawaelezea wale wanao pendana kama watu wanao tembea katika utiifu. Tunatii amri za Yesu kwa kiwango gani na upendo wetu unatoka kwa tamaa zetu za ubinafsi au kutoka kwa mioyo yetu mtiifu?
3. Tunajuaje kama mtu ni 'mdanganyifu na mpinga Kristo', anavyo elezea katika waraka huu?
4. Ni kwa njia zipi tunakuwa waangalifu juu ya wale ambao wanaweza kuleta mafundisho ya uwongo katika kanisa letu na maisha yetu?
5. Unachukulia sana ushirika wa ana kwa ana?